TANGAZO LA SERIKALI NA. 310 la tarehe 26/4/2024

SHERIA YA KODI YA MAPATO,

(SURA YA 332)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya Kifungu cha 10)*

AMRI YA MSAMAHA WA KODI YA KODI YA ZUIO KATIKA MRADI WA UKAMILISHAJI WA KAZI ZA UKARABATI WA MTAMBO WA KUSAFISHIA MAJI KATIKA MITAMBO YA WAMI- CHALINZE, UJENZI WA MTANDAO MKUBWA NA MDOGO WA BOMBA LA USAMBAZAJI MAJI NA UJENZI WA TENKI KUU ZA KUHIFADHIA NA KUSAMBAZA MAJI KATIKA VIJIJI VYA CHALINZE KWA KAMPUNI YA AFCONS INFRASTRUCTURES LIMITED YA MWAKA 2024

Jina na kuanza kutumika

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Kodi ya Zuio kwenye Mradi wa Ukamilishaji wa Kazi za Ukarabati wa Mtambo wa Kusafishia Maji Katika Mitambo ya Wami- Chalinze, Ujenzi wa Mtandao Mkubwa na Mdogo wa Bomba la Usambazaji Maji na Ujenzi wa Tenki Kuu za Kuhifadhia na Kusambaza Maji katika Vijiji vya Chalinze kwa kampuni ya Afcons Infrastructures Limited ya Mwaka 2024 na itachukuliwa kuwa ilianza kutumika tangu tarehe 26 Februari, 2024.

Msamaha

2. Kodi ya Zuio inayotokana na Kampuni ya Afcons

Infrastructures Limited katika utekelezaji wa Mkataba kati ya Dar es Salaam Water Supply and Sanitation Authority na kampuni ya Afcons Infrastructure Limited kwa ajili ya Mradi wa Ukamilishaji wa Kazi za Ukarabati wa Mtambo wa Kusafishia Maji Katika Mitambo ya Wami- Chalinze, Ujenzi wa Mtandao Mkubwa na Mdogo wa Bomba la Usambazaji Maji na Ujenzi wa Tenki Kuu za Kuhifadhia na Kusambaza Maji katika Vijiji vya Chalinze kwa kampuni ya Afcons Infrastructure Limited , ya kiasi cha shilingi 1,336,477,876.50 kimesamehewa.

Ukomo

3. Amri hii itafika ukomo wake baada ya Kampuni ya Afcons Infrastructure Limited kuondolewa wajibu wa kulipa shilingi 1,336,477,876.50 utokanao na Mkataba ulioingiwa chini ya aya ya 2.

Dodoma,
8 April, 2024

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
*Waziri wa Fedha*